

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MAKANJIRO,
S.L.P 116,
RUANGWA
TAREHE.....**

JINA LA MZAZI/MLEZI.....

S.L.P 51

RUANGWA

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI
MAKANJIRO ILIYOPO KATA YA MAKANJIRO WILAYA YA RUANGWA KWA
MWAKA.....**

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka.....

Shule ya sekondari Makanjiro ipo umbali wa km 10 kutoka halmashauri ya wilaya ya ruangwa kuelekea wilaya ya Nachingwea, kandokando ya barabara itokayo kijiji cha Mmawa likunja kuelekea kijiji cha rewje umbali wa mita 200.

Shule hii ni ya kutwa kwa wavulana na wasichana. Unatakiwa kumripotisha shuleni mwanao tarehe..... siku ya kufungua shule na mwisho kuripiti ni tarehe.....ni muhimu siku ya kufungua shule awepo shuleni

MAAGIZO MUHIMU KWA MWANAFUNZI

1. SARE ZA SHULE WAVULANA

- Suruali rangi ya damu yam zee (maroon) mbili (mshono wa suruali uwe na rinda 2 kila upande
- Mashati meupe mikono mifupi mawili
- Tai rangi ya damu yam zee (maroon)
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vya kufunga na Kamba
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Mkanda mweusi
- Tshirt za shule rangi ya bluu kama sare ya shule

- Sare kwa ajili ya michezo (jezi rangi nyeusi)

WASICHANA

- Sketi rangi ya damu yam zee mbili (mshono wa rinda box)
- Mashati meupe mikono mifupi mawili(ila kwa watakaovaa hijabu watashona nusu kanzu)
- Tai rangi ya damu yam zee (maroon)
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vya kufunga na Kamba
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Hijabu kwa wanafunzi wa kiislamu inatakiwa ifanane na sare za shule
- Sare kwa ajili ya michezo (jezi rangi nyeusi)

N:B Sare za shule ni lazima ziwe zenye heshima kwa kuzingatia ushonaji kwani zisiwe fupi, za kubana au modo kwa wavulana. Yeboyabo na vibajaji haviruhusiwi, kwenda kinyume na hivyo ni kukiuka sheria za shule

2. MAHITAJI YA TAALUMA

Mwanafunzi anatakiwa kuja na ;-

- Daftari 10 (counter book quire 2 au 3 au zaidi)
- Kalamu,rula,begi la daftari, peni na mkebe
- Aje na fomu ya afya iliyojazwa na daktari wa wilaya ambayo imeambatanisha pamoja na fomu hii ya kujiunga
- Kamusi ya Kiswahili na kingereza (DICTIONARY)

3. VIFAA VYA USAFI

Vifaa hivi afike navyo siku ya kufungua shule vikiwa vipya na vimenolewa

- Ndoo ndogo ya lita kumi
- Jembe
- Panga
- Kwanja(fyekeo)

NB:

- Fomu ya kwenda hospitali imeambatanishwa nyuma ya fomu hii ya maelekezo
- Sheria na kanuni za shule pia zimeambatanishwa nyuma ya fomu hii

Nikutakie maandalizi mema ya mwanao